

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**  
**21 Machi 2009**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Ally Saidi Mwisheshe  
Bashiri Rashidi  
Beda John Mkusu  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Frank Peter Rwechungura  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Juma Ali Salehe Jongo  
Mejah Mbuya  
Paulo Atibu Hatibu  
Rashidi Saidi Karanji  
Shamte J Kigoma  
Sosthenes C Amlima  
Sudi Saidi Ramadhan

**Mkutano na serikali ya jiji**

Jumatano tarehe 18 Machi, Mejah, Elaine, Juma, Paulo na Filbert walikutana na idara ya mipango miji, mazingira na usafiri ya serikali ya jiji. Tulikutana na Bwana Chirstopher Japhet, mkuu wa idara, Ms Neema Kinyago, Ms Ester Mijinga na Ms Martha Mkapasi mkuu wa mradi wa mijii salama. Tulitambulisha UWABA, faidha za baisikeli kama chombo cha usafiri na mafanyakyo ya UWABA. Tulieleza matatizo tumepata kuwasiliana na idara nyingi za serikali na pendekezo letu la Kongamano kuhusu usafiri wa siyo ya moto. Washiriki wawe Wizara ya Miundumbinu, TANROADS, serikali ya jiji, serikali za manispaa na traffic police. Walipenda wazo hili na walisema itasaidia kuwa na uratibu. Walisema wapo tayari kuomba mkurugenzi kuandika barua za kualika washiriki. Walipendekeza washiriki wengine kama wizara ya ardhi na chuo cha ardhi. Tulisema ubalozi wa uholonzi walisema watatoa ukumbi na chakula. Waliuliza kama posho zipo humu. Tulisema ubalozi wa uholonzi walisema hawawezi kutoa posho. Walisema mkurugenzi hatakuwa tayari kualika washiriki kama posho haipo ya Tsh 20,000 mpaka Tsh 30,000 kwa mtu. Tulikubali kuomba ubalozi wa uholonzi, benki ya dunia na JICA kulipa posho hizi.

Leo kwenye mkutano wa UWABA tulizungumza kuhusu hiyo. Tunasikia kwa nini watu wa serikali hawafanyi kazi bila posho hata kama wanapata mshahara wakati sisi wanachama tunafanya kazi bila msharaha wala posho. Kazi ya uratibu ni kazi ya serikali ya jiji. Pia wao hawajasema kama watatafuta hela kutoka badjeti yao.

Baada ya mkutano na serikali ya jiji Elaine alitumia email kwa Dieter Schelling wa World Bank na Stefan Hulitz wa ubalozi wa uholonzi kueleza shida lakini wote hawapo ofisini wiki hii. Pia alitembelea JICA na mtu anayehusika (Asuke Tsuboike) hakuwepo. Tulikubali kuandika barua kuomba mkutano na JICA.

### **Mradi wa Wamba**

Una Osili alijibu kwamba atafuatalia kupata karatasi inayoonyesha hela imekuwa transferred.

### **Ushirika wa kibarua cha baiskeli**

Elaine alitembelea ofisa wa ushirika wa mkoa nwa ushirika wa wilaya Kinondoni Bwana Bukuku. Wasaidizi wa Bwana Bukuku walikata tamaa lakini baada ya maelezo marefu kwa Bwana Bukuku alisema tuandike barua kuomba usajili na tutafute sehemu ya mkutano kama shule na wao watakuja kufanya mkutano wa taarifa kutuelimisha kuhusu vipi kuanzisha na kutawala ushirika . Edgar alikubali kupeleka barua.

Tulikubali jina kwa ushirika - “Fasta bicycle messengers”. Tulikubali watu wengine watakuwepo mjini kusubiri kazi na kusambaza vipeperushi na mtu mmoja atakuwa na simu ya ushirika. Tutagawana faidha kwa kulingana na masaa ya kazi - kazi ya mjini itakuwa thamani mara mbili ya kazi ya kujibu simu. Tulikubali kutengeneza badjeti baada ya mkutano wa taarifa.

### **Ruzuku ya Foundation for Civil Society**

Elaine anafuatalia kupata CVs ya waaalimu wa kompyuta.

### **Video ya usalama wa baiskeli**

Elaine alipata software kutengeneza DVDs. Atatengeneza DVDs na pia CDs. Mejah atachangia DVDs.

### **Juma**

Juma amehamisha vitu vyake kutoka ofisi.

### **Mashindano ya wimbo**

Mejah, Sosthenes na Edgar watatafuta gharama za kutengeneza single.

### **Mkutano wa WHO**

Tumealikwa kwenye mkutano wa usalama wa barabarani ya shirika la dunia la afya (WHO) ubeliji. Jina la Elaine alikuwa kwenye barua lakini aliomba wanachama wa Tanzania wahudhurie. Bado hawajajibu email. Tulifanya orodha ya wanachama wa UWABA ambao wana passport na wanaojua kiingereza - Mejah, Filbert, Sosthenes na Edgar. Elaine atafuatalia kujua kuna nafasi ngapi kwa wanachama wa UWABA.

### **Hela na guta**

Filbert anadaiwa Tsh 14,000 ya hela ya guta. Juma ana Tsh 7,000 ya hela ya UWABA. Ali Saidi Mwishehe anadaiwa Tsh 21,000.

**Kufika mapema**

Tulikubaliana tufike mapema kwenye mikutano.